MAWASILIANO

LUGHA

Lugha ni nini?

Lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zenye kubeba maana zilizokubaliwa na jamii ya watu fulani ili zitumike katika mawasiliano.

- Lugha ndio nyenzo kuu ya mawasiliano baina ya binadamu na binadamu.
- Kimsingi lugha hutumia sauti zenye maneno ambayo yamepangiliwa kwa njia maalumu ili kuleta maana iliyo kusudiwa.
- Binadamu hutumia lugha ili kukidhi mahitaji yake ya kila siku, watu hutumia lugha kupashana habari, kubadilisha mawazo.
- Ili mawasiliano yawepo, mpangilio wa maneno huna budi kuleta maana.
- Lugha hutofautiana kulingana na watumiaji.

Mfano:

- Kihaya ni lugha inayotumika na wahaya
- Kibena ni lugha inayotumika na wabena
- Kijerumani ni lugha inayotumika na wajerumani

Lugha hujengwa kwa maneno, maneno hujengwa kwa vitamkwa vyenye mpangilio maalum ambao hulipa neno maana. Maneno yakipangwa kwa njia maalum hutoa kauli zenye maana. Hivyo lugha ili iweze kuleta mawasiliano baina ya wazungumzaji muundo wake huanzia vitamkwa, maneno na hata kauli hupangiliwa kwa njia maalum.

Mfano:

Vitamkwa: - chu, ch, k,a,l,u,o vitamkwa hivi hujenga maneno- chakula, chuo nk.

Katika lugha ya kiswahili vitamkwa hukamilishwa kwa kutumia herufi za alfabeti. Alfabet zimegawanyika katika konsonati na irabu

Konsonati: - b,c,d,f,g,h,j,k,l,m,n,p,q,r,s,t,v,w,x,y,z.

Irabu: -a,e,i,o,u

Kutokana na alfabeti hizi lugha ya kiswahili imejenga maneno mbalimbali ambayo ndio msingi wa mawasiliano kwa watanzania na mataifa mengine.

- Mawasiliano yasiyotumia sauti sio lugha kwa sababu hapo hutumii sauti wala maneno vilevile mawasiliano ya wanyama, wadudu hayawezi kuitwa lugha kwa sababu hiyohiyo.

LUGHA FASAHA

Ni lugha ambayo inafuata taratibu zote za lugha hiyo yaani , kimaana, kimuundo kimatamshi na kimantiki.

Ili mawasiliano yawe mazuri, wazungumzaji watumie lugha fasaha.

(a) Maana: -

Ili lugha iwe fasaha katika misingi ya maana au msamiati uliokusudiwa, mfano neno barabara lina maana mbili. Mtu anaweza kukosea badala ya kusema njia akasema sawasawa.

(b) Muundo: -

Ufasaha wa lugha hujitokeza kutokana na mpangilio wa maneno kuwa mzuri,

Mfano: - kikubwa kitabu badala ya kitabu kikubwa

(c) Matamshi: -

Download more free notes and revision materials at www.teacher.ac

Sauti za lugha yoyote ile zitamkwe kama zinavyotakiwa ili kujenga ufasaha katika lugha hiyo.
Mfano baadhi ya watu hushidwa kutamka baadhi ya maneno
Mfano: **zamb**i badala ya **dhambi**
Zarura badala ya **dharura**

(d) Mantiki
Ili maana iliyolengwa iweze kuwepo kauli lazima ziwe na mantiki
Mfano: Nimemkuta hayupo **badala ya** sijamkuta
Chai imeingia nzi **badala ya** inzi ameingia kwenye chai

ATHARI ZA KUTOTUMIA LUGHA FASAHA
Lugha isipotumika kwa ufasaha
(i) Yaweza kukwamisha mawasiliano
(ii) Lugha hiyo kukosa hadhi na kuonekana kama ya wahuni

AINA ZA MANENO

NENO

Sio rahisi kufasiri neno, kutokana na ukweli huo neno limeelezwa kwa namna nyingi tofautitofauti. Mathalani wanasarufi mapokeo wanaeleza maana ya neno kwa kuangalia uhusiano wa maneno katika tungo. Hivyo wanasema neno ni tamko lenye kubeba maana ambalo hutengwa kwa nafasi kati ya neno na neno jingine.

Wanamuundo wanaeleza kuwa neno ni tamko lolote lenye kuleta maana na ambalo pia laweza kuleta jibu la swali mfano je umekula? La! kwahiyo "la" ni tamko ambalo lina hadhi ya kuwa neno.

Kwa sarufi mapokeo maneno yamefasiriwa kwa kuangalia maana ya maneno hayo, uhusiano wa maneno hayo na mengine katika tungo.

Wanamuundo wanafasiri maneno na aina zake kwa kuangalia muundo wa maneno hayo na tabia zake katika tungo pamoja na hayo mbinu za sarufi mapokeo hutumika hapa na pale.

1. Nomino
2. Viwakilishi
3. Vivumishi
4. Vitenzi
5. Vielezi
6. Viunganishi
7. Vihisishi

1. **NOMINO**

Nomino ni maneno yanayotaja majina ya watu, wanyama, mahali, vitu n.k. Tabia zake kimuundo ni maneno yanayochukua viambishi, ngeli ambavyo pia vinaonyesha idadi. Aidha Nomino ni maneno makuu yanayotawala kirai nomino, mfano jua,Seif, Morogoro n.k.

AINA ZA NOMINO

(a) Nomino za pekee

Ni maneno yanayotaja watu, mahali, maumbile mbalimbali ya kijiografia n.k. angalau maneno haya yanapoandikwa huanzia na herufi kubwa mfano: Nyerere, Ali, Singida, Nile n.k.

(b)Nomino za kawaida

Ni maneno yanayotaja vitu vyenye tabia za kifaradhi (universal) mfano: mtoto, mtu, nyumba, baba n.k.

(c) Nomino za jumla

Nomino zinazotaja vitu katika uwingi wake mfano jeshi, mchunga, kundi, jamii n.k

(d)Nomino dhahania

Nomino zinazotaja vitu visivyoweza kuonekana au kushikika aghalabu vitu hivi huwa vya kifikra au kusadikika mfano, njaa, furaha, upepo zimwi n.k

2. **VIWAKILISHI**

Ni maneno ambayo hutumika badala ya nomino ambayo yanatabia zilezile za kinomino mfano kutawala kirai nomino na kuchukua viambishi ngeli mfano, wewe, sisi n.k.

AINA ZA VIWAKILISHI

(a) Viwakilishi nafsi – hivi ni viwakilishi ambavyo hubainisha nafsi za wazungumzaji

(i) Viwakilishi nafsi huru ni maneno kamili mfano: -

UMOJA		**WINGI**
Nafsi I	Mimi	sisi – Mzungumzaji
Nafsi II	wewe	ninyi/ nyinyi – msikilizaji
Nafsi III	yeye	wao – mzungumzaji

Download more free notes and revision materials at www.teacher.ac

(ii) Viwakilishi nafsi viambata – hivi vipo katika umbo la mofimu na huambatanishwa na vitenzi mfano: -

UMOJA		**WINGI**
Nafsi I	Ninakuja	Tunakuja
Nafsi II	Unakuja	mnakuja
Nafsi II	Anakuja	wanakuja

(iii) Viwakilishi vya kumiliki

Hubainisha dhana ya kumiliki

Mfano: angu, enu, ako, ake n.k

(iv) Viwakilishi vya kuuliza

Hivi hudokeza maswali

Mfano: kipi, gani, epi n.k

(v) Viwakilishi vya kuonesha

Mfano: huyu, hawa, zile, kile, hiki n.k

(vi) Viwakilishi vya msisitizo;- ndi - na - amba- - mfano ndiye, ndiwe, ambaye, ambalo n.k

- Viwakilishi vya kumiliki, kuuliza na kuonesha hutumika kama vivumishi iwapo vitaambatana na nomino

Mfano:

- Mtoto wangu sijamuona
- Mtoto wako amefika wangu hajaonekana bado

Wakati mwingine kiwakilishi huweza kuwa nomino, kiwakilishi au kitenzi

Mfano: -

- Kiti kizuri kimevunjika
- Kizuri kimevunjika

Download more free notes and revision materials at www.teacher.ac
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

o Anacheza vizuri

3. **VIVUMISHI (V)**

Kimapokeo vivumishi ni maneno ambayo yanaambatana na nomino au viwakilishi yakitoa taarifa juu ya nomino au viwakilishi hivyo.

Katika sarufi muundo vivumishi ni maneno yanayochukua viambishi ngeli kama ilivyo katika nomino na aidha ni maneno yanayotawala kirai vumishi.

Mfano:-

Mkubwa, kubwa,kikubwa. Viambishi awali ni viambishi ngeli

AINA ZA VIVUMISHI

Muainisho wa vivumishi hutegemea zaidi dhima ya kisemantiki katika tungo. Kwa mfano kisemantiki vivumishi vyaweza kuwa vyakueleza namna au jinsi idadi, kuuliza n.k.

(i) Vivumishi vya sifa

Kwa kiasi kikubwa hivi hueleza namna au jinsi ya nomino au kiwakilishi mfano: -

(a) Vivumishi halisi: - Hivi havichukui viambishi ngeli mfano: hodari

(b) Vivumishi visivyo halisi: - mfano hivi ni vile vinavyochukua viambishi ngeli – pole, - kubwa, ... n.k

(ii) Vivumishi vya kuuliza

Ni vivumishi vinavyodokeza swali mfano:

- Mtoto yupi?
- Nyumba gani?

(iii) Vivumishi vya kumiliki

Hivi hujenga dhana ya umilikaji mfano:

- Kiti changu
- Kazi zetu
- Tabia yako

(iv) Vivumishi vya kuonesha

Hivi hudokeza umbali au ukaribu wa nomino mfano:

- Nyumba hii
- Watoto wale

(v) Vivumishi vya idadi

Ni vivumishi vinavyodokeza idadi katika dhana ya umoja au wingi mfano:

- Watoto wawili
- Watu wengi
- Maji kidogo

(vi) Vivumishi vya jina kwa jina

Vivumishi vya aina hii ni nomino ambazo huwa na dhima ya kuvumisha nomino au kiwakilishi mfano:

- Mwalimu Zakia
- Baba Juma

(vii) Vivumishi vya –A- unganifu

Ni vivumishi vinavyojenga dhana ya kimilikisho ambayo hujengwa na j=kiambata –a- kinachochukua kiambishi ngeli kadiri ya nomino milikishwa mfano:

- Nyumba ya baba
- Kitenge cha mama

(viii) Vivumishi vya –enye-, -enyewe- mfano:

- Mtoto mwenye
- Nyumba yenye
- Mtoto mwenyewe
- Nyumba yenyewe

(ix) Vivumishi vya o-te-

Mfano: -

- Nyumba yoyote
- Kiwanja chochote

(x) Vivumishi vya– ingine –engine

Mfano:

- Kiti kingine

- Watu wengine

4. **VITENZI**

Kimapokeo vitenzi ni maneno yanayoeleza jambo linalotendwa na nomino au hali ya nomino mfano:

(a) Juma anacheza mchezo

(b) Juma ni mgonjwa

Kimuundo vitenzi ni maneno yanayounda kirai tenzi na aidha huchukua vipatanisho vya kisanifu vilevile vina uwezo wa kujenga dhana mbalimbali mfano: njeo, haki tofauti, kauli tofauti tofauti n.k

Mfano :-

- Mtoto anacheza
- Watoto wanacheza

AINA YA VITENZI

Katika sarufi mapokeo vitenzi ni vya aina tatu,

(i) vitenzi vikuu (T)

(ii) vitenzi visaidizi (TS)

(iii) vitenzi vishirikishi (t)

kwa sarufi muundo vitenzi ni vya aina mbili

(a) vitenzi halisi

Hivi vina sifa kamili ya kileksika vinasimama peke yake na kuunda KT yaani kirai tenzi (T), mfano: mtoto kaja , wale wanalia

T T

(b) Vitenzi vipungufu: - (visivyo halisi)

Hivi ni vitenzi ambavyo havina hadhi kubwa kama vitenzi halisi.

Kimapokeo vinaitwa vitenzi visaidizi kazi yake kubwa ni kusaidia vitenzi vikuu kujenga dhana au maana ya ziada kuhusiana na kitenzi kikuu

mfano:- Ndege alikuwa anacheza

Ts T

VITENZI VISHIRIKISHI (t)

Hivi ni vitenzi vipungufu na dhima yake ni kuonesha uhusiano baina ya nomino au kiwakilishi na maneno mengine katika tungo mfano: nomino, kiwakilishi, kivumishi au kitenzi.

Mfano: -

Juma ni mchezaji

t

juma ndiye wewe

t

Mtoto alikuwa hodari

t

Mtoto yumo ndani

t

AINA ZA VITENZI VISHIRIKISHI

Vitenzi vishirikishi ni vya aina tofautitofauti kutegemea dhana inayobebwa na vitenzi hivyo kisemantiki

(a) Vitenzi vya KUWA

Mfano: hali yakinishi kanushi

(i) Alikuwa hakuwa

(ii) Ni si

(iii) Atakuwa hatakuwa

(b) Vitenzi vya kuwa NA

Ni vitenzi vinavyojenga dhana ya kumiliki mfano

(i) Mama alikuwa na nyumba

(ii) Mama ana nyumba

(iii) Mama atakuwa na nyumba

(c) Vitenzi vya mofimu – PO- , - MO -, - KO-.

Mfano:-

(i) Simba yupo ndani

(ii) Mtoto yumo ndani

(iii) Mtoto yuko nje

(d) Vitenzi vya msisitizo NDI

Mfano: -

(i) Huyu ndiye Juma Huyu siye

(ii) Wewe ndiwe Juma sisi ndio wenyewe

(e) Vitenzi vya msisitizo AMBA

Mfano:

(i) Huyu ambaye yupo

(ii) Hawa ambao wapo

5. **VIELEZI**

Vielezi ni maneno ambayo ni vigumu kuyafasihi moja kwa moja isipokuwa yanafasihika kutokana na tabia zake na jukumu la kimantiki katika TUNGO.

Mfano: - kuna vielezi vinavyoeleza juu ya kivumishi, vingine juu ya vitenzi na kielezi kingenecho.

(a) Mtoto mwema sana

(b) Mtoto anakuwa taratibu

(c) Mtoto anakuwa taratibu mno

AINA ZA VIELEZI

Pamoja na kwamba vielezi vina tabia ya kuhamahama, kudondosheka katika tungo pia vinajibu maswali kadhaa katika tungo. Kutokana na maswali yanayojibiwa na vielezi ni vya aina nne.Mfano: -

(a) Vielezi vya namna au jinsi

Mfano: mtoto anatembea polepole

Anaongea kinyumenyume

(b) Vielezi vya mahali (wapi)

Mfano: - Mbwa alibweka magengeni

(c) Vielezi vya idadi au kiasi (mara ngapi kwa idadi gani)

Mfano: - wanacheza mara kwa mara

(d) Vielezi vya wakati (lini)

Alionekana juzi

Pamoja na idadi hii ya vielezi kuna vielezi vya ziada

Mfano:- vielezi vya kasoro au upungufu, vya sababu, vya hali ya masharti n.k

6. **KIUNGANISHI (U)**

Haya ni maneno yanayojenga dhana ya uunganikaji baina ya neno na neno, kirai na kirai, kishazi na kishazi, sentensi na sentensi

Mfano:- na, ila, bali, pia, ama, au, pamoja na alama ya koma.

7. **VIHISISHI (H)**

Haya ni maneno yanayodokeza vionjo vya moyo, yanaponukuliwa yanaambatana na alama ya mshangao, yala! Oye! Oh! Masalale! Lahaulaa, Alaa!!

MATUMIZI YA KAMUSI

Kamusi;- Ni kitabu cha maneno yaliyopangwa kwa utaratibu wa kialfabeti na kutolewa maana na maelezo mengine. Kitabu hiki huwa na idadi kubwa ya maneno kutoka katika lugha husika, na maneno hayo hutolewa maana na maelezo kwa lugha hiyohiyo au kwa lugha nyingine.

MUUNDO WA KAMUSI

Kamusi yoyote ile imegawanyika katika sehemu tatu nazo ni;-

a) Mwongozo wa msomaji (Utangulizi wa kamusi)

b) Vifupisho na matumizi ya alama

c) Kamusi yenyewe (matiri ya kamusi)

a) Mwongozo wa msomaji

Ni usuli ambao unalenga kumuelekeza mtumiaji wa kamusi ili aweze kutumia kamusi hiyo bila kupata usumbufu. Muongozo wa msomaji huhusika na mambo yafuatayo;-

i) Taarifa zilizoingizwa kam vile;
- Vidalizo.
- Vibadala vya vidalizo.

ii) Kategoria ya maneno
- Nomino
- Vitenzi
- Vielezi
- Vivumishi
- Umoja na wingi n.k

iii) Maneno na utumizi wa maneno
mfano;- Nomino (sarufi)
- Elementi (kemia)

iv) Mifano ya matumizi

v) Lugha kienzo.

b) Ufupisho wa matumizi ya alama

Ni muhimu kwa mtumiaji wa kamusi kupata taarifa zinazohusu matumizi mbalimbali ya vifupisho , tarakimu, herufi na maana.
Mfano;- agh - aghalabu
ele - elekeza
fiz - fizikia
Kb - kibaharia
Kd - kidini
Kh - kihusishi
K.v - kamavile
Kv - kivumishi
Mt - methali

nh - nahau
n.k - Na kadhalika

c) Kamusi yenyewe

Hii ni sehemu ambayo inakuwa na orodha ya maneno mbalimbali yenye maana na ufafanuzi wa neno husika. Sehemu hii ndio kiini cha kamusi.

UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU KATIKA MADA HII YA UTUMIZI WA KAMUSI

Ni vema kufahamu istilahi kuu katika kujadili mada hii. Istilahi hizo ni hizi zifuatazo;

i) Kidahizo

ii) Kitomeo

iii) Lugha kienzo

i) KIDAHIZO
Kidahizo ni neno lilioingizwa katika kamusi ili lipatiwe maana na ufafanuzi mwingine wa kisarufi (kimatamshi, kimuundo) na kimatumizi. Vidahizo huandikwa kwa kukolezwa wino. Mfano;- **abee! bee!** (kwa wanawake) neno la kuitika wanapoitwa.

Mpangilio wa vidahizo
Kutokana na tofauti za kimuundo katika aina moja ya neno na aina nyingineya neno kikategoria, vidahizo huwekewa utaratibu maalum katika kuingiza vidahizo hivyo. Jambo la msingi kuelewa ni kwamba ,vidahizo hupangwa kwa kufuata utaratibu wa kialfabeti.

ii) KITOMEO
Kitomeo ni kidahizo na maelezo yake yote. Au kitomeo ni neno lililoingizwa katika kamusi kama kidahizo pamoja na taarifa zake zote. Kwa mfano;-

Kitomeo cha 1. **Maalimu** - Ni mtu mwenye elimu kubwa ya dini ya kiislamu.

Kitomeo cha 2. **aathari** - Ni masalio ya vitu na utamaduni wa watu fulani.

Kitomeo cha 3. **abaa!** - Neno la kumwita rafiki, alaa! Aisee!

Kitomeo cha 4. **abadani!** Ni neno linalosisitiza jambo la ufupi, ufasaha, utoshelevu na uwazi . Mtindo huu hutumia alama zinazofupisha maelezo marefu au fasihi mbalimbali.

iii) LUGHA KIENZO
Ni mtindo unaotumika kutolea fasihi za vidahizo katika kamusi kwa ufupi, ufasaha, utoshelevu na uwazi. Mtindo huu hutumia alama zinazofupisha maelezo marefu au fasihi mbalimbali.

FASIHI KWA UJUMLA

Fasihi:

Ni sanaa inayotumia lugha ili kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa .

Ni sanaa kwa sababu huumbwa kwa lugha katika hali ya kuvutia na kuweka madoido ya kila namna ili iweze kuvutia wasomaji au wasimuliaji wake, lengo lake kuu ni kufikisha ujumbe kwa jamii.

SANAA

Ni uzuri unaojitokeza katika umbo lililosanifiwa, umbo ambalo mtu hulitumia kueleza hisia zinazomgusa kwa kutoa kielelezo chenye maana. Hivyo unaona kazi za sanaa katika nyanja mbalimbali kama vile: -

- Utarizi

- Fasihi

- Ushonaji

- Muziki

- Ususi

- Ufumaji uchoraji



DHIMA ZA FASIHI

(i) Kusisimua

(ii) Kuhifadhi na kurithisha amali za jamii

(iii) Kudumisha na kuendeleza lugha

(iv) Kuelimisha jamii

(a) KUSISIMUA

Hujikita zaidi katika mpangilio wa maneno lugha ya picha mandhari, tamathali au semi

Mfano: -

Ndugu yetu ametutupa mkono (amefariki)

Sentensi inajaribu kutuliza uchungu na hivyo kuleta faraja.

(b) Kuhifadhi na kurithisha amali za jamii

Fasihi huhifadhi na kutunza mila na desturi za fani na pia huweza kurithisha mila hizo kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

(c) Kudumisha na kuendeleza lugha

Kwa kadri lugha inavyotumiwa na watumizi, maneno yalivyobuniwa na kuenezwa zamani, leo yanatumiwa na watunzi wa mashairi, kwaya , nyimbo n.k

(d) Kuelimisha jamii

Fasihi hukosoa, huonya na kurekebisha jamii hueleza waziwazi wale wanaotenda kinyume na matakwa ya jamii, inabidi kukemea na kuonyana kwa kutumia methali, nahau

Mfano: - Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

Hii inatoa tahadhari

AINA ZA FASIHI

Kuna aina mbili (2) za fasihi

(a) Fasihi andishi

(b) Fasihi simulizi

1. **FASIHI SIMULIZI**

Ni fasihi ambayo hutumia masimulizi ya mdomo kufikisha ujumbe wake kwa jamii.

Ni fasihi ambayo ni kongwe na ilianza tangu binadamu alipoanza kuishi duniani.

FASIHI SIMULIZI INA TANZU NNE NAZO NI

(i) Hadithi

(ii) Semi

(iii) Ushairi

(iv) Maigizo

2. **FASIHI ANDISHI**

Ni fasihi ambayo hutumia maandishi ili kufikisha ujumbe kwa jamii

Fasihi andishi ina tanzu nne

(i) Tamthilia

(ii) Ushairi

(iii) Ngonjera

(iv) Riwaya

TOFAUTI KATI YA FASIHI SIMULIZI NA FASIHI ANDISHI

NA	FASIHI SIMULIZI	FASIHI ANDISHI
1	Huwasilishwa na fanani kwa njia ya masimulizi au mdomo	Huwasilishwa kwa maandishi kwa njia ya maandishi
2	Huifadhiwa kichwani na kusambazwa na mdomo au mazungumzo	Huifadhiwa kwa maandishi na kusambazwa kwa maandishi
3	Huruhusu mabadiliko ya papo kwa papo	Hairuhusu mabadiliko ya papohapo kazi ikishaandikwa haibadiliki hadi toleo jingine
4	Ina tanzu nne kama vile	Ina tanzu tatu kama vile

	- Hadithi - Semi - Sanaa za maonesho maigizo	- Ushairi - Tamthilia - Riwaya
5.	Hadhira yake ni watu wale katika jamii - Watoto - Wazee - Wasomi	Hadhira yake ni watu wale wanaojua kusoma na kuandika
6	Inaumri mkubwa	Ina umri mdogo imekuwepo baada ya ugunduzi wa maandishi
7	Ni rahisi kusahau baadhi ya vipengele	Si rahisi kusahauliwa baadhi ya vipengele kwani imehifadhiwa kwa maandishi.
8	Muundo wake ni wa moja kwa moja	Mara nyingi muundo wake ni wa mchangamano unaruhusu urejeshi
9	Huenda na wakati na mabadiliko ya matukio katika jamii	Haiendi na wakati kwa sababu ikishaandikwa haiwezi kubadilishwa.

TANZU ZA FASIHI SIMULIZI

Fasihi simulizi hujitokeza katika tanzu kuu nne, ambazo ni hadithi, semi, ushairi, na maigizo. Tanzu hizi zinaweza kuoneshwa katika mchoro ufuatao na vipera vyake



HADITHI

Ni tungo za fasihi simulizi zitumiazo lugha ya ujazo na maongezi ya kila siku.

Masimulizi huwa ni mafupi yaliyopangwa katika mtiririko unaokamilisha visa.

VIPERA VYA HADITHI

(i) Ngano

(ii) Tarihi

(iii) Vigano

(iv) Soga

NGANO

Hizi ni hadithi zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu kuelezea au kuonya.

TARIHI

Ni hadithi ambazo husimulia kuhusu matukio ya kihistoria, matukio hayo yanaweza kuwa ya kweli au ya kubuni.

VIGANO

Ni hadithi fupi zinazoelezea makosa au uovu wa watu fulani na kueleza maadili yanayofaa. Vigano hutumia methali kama msingi wa maadili yake.

SOGA

Ni hadithi fupi za kuchekesha na kukejeli. Wahusika wa soga ni watu wa kubuni. Soga husema ukweli unaohimiza lakini ukweli huo hujenga vichekesho ili kupunguza makali.

USHAIRI

Ushairi katika fasihi simulizi ni fungu linalojumuisha tungo zote zenye kutumia mapigo ya sauti kwa utaratibu maalumu

VIPERA VYA USHAIRI

(i) Mashairi

(ii) Utenzi

(iii) Nyimbo

(iv) Ngonjera

MASHAIRI

Ni tungo zenye mpangilio maalumu wa silabi na lugha ya mkato.

UTENZI

Ni tungo ndefu ya kimasimulizi au kimawaidha utenzi kutofautiana na ushauri kwa kuwa na mistari mifupimifupi isiyozidi mizani.

NYIMBO

Ni tungo zenye mpangilio maalumu wa maneno na mahadhi yaani hupenda kuimbwa na kuambatana na ala za muziki au sanaa.

NGONJERA

Zina muundo wa mashahiri ya kimapokeo na huwa katika muundo wa mazungumzo baina ya watu wawili au makundi ya watu wanaolumbana na mwishowe kufikia mwafaka/ suluhisho.

SEMI

Ni tungo za fasihi simulizi ambazo ni fupi na zenye kutumia lugha ya picha.

VIPERA VYA SEMI

(i) Methali

(ii) Mafumbo

(iii) Nahau

(iv) Vitendawili

METHALI

Ni misemo ambayo hutoa hekima na busara kwa kuundwa kwa mpangilio wa pande mbili za fikra

Mfano: -

- Kidole kimoja hakivunji chawa

- Haba na haba hujaza kibaba

MAFUMBO

Ni kauli zinazoeleza maana waziwazi na kutumia maficho

Mfano:-

- Hakamatiki hashikiki (moshi)

- Uzalendo umemshinda (umeshindwa kuvumilia)

KITENDAWILI

Ni usemi uliofumbwa hutolewa kwa hadhira, ufumbuliwe, kitendawili kufanya kazi ya kumfikisha msikilizaji.

Mfano: -

Uzi mwembamba umefunga dume (usingizi)

NAHAU

Ni kauli zilizojengwa kwa picha kwa kutumia maneno ya kawaida lakini zinatoa maana isiyo ya kawaida.

Mfano: -

- Amepata jiko (ameoa)

- Ana mkono mrefu (mwizi)

- Ana mkono wa birika (mchoyo)

- Amevaa miwani (amelewa)

MAIGIZO SANAA ZA MAONYESHO

Ni masimulizi yenye utendaji ambayo huonesha mambo yaliyotokea, yatakayotokea lengo ni kufikisha ujumbe.

VIPERA VYAKE NI:-

(i) Michezo ya kuigiza

(ii) Majigambo

(iii) Ngonjera

(iv) Vichekesho

MICHEZO YA KUIGIZA

Ni maigizo marafu ya visa vinavyowakilisha maisha ya jamii fulani. Michezo mingine huafiki na mingine hulaani mambo yasiyofaa, michezo ya watoto wadogo pia huwasaidia kujifunza maadili ya jamii hiyo.

MAJIGAMBO

Ni maigizo ya kujitapa /kujigamba kutokana na kuweza kufanya jambo la kishujaa au lisilo la kawaida. Mtambaji husimulia na kutenda akionyesha jinsi alivyofanya jambo lile.

Mfano: -

Askari aliyerudi vitani,mtu aliyemuua simba n.k

NGONJERA

Ni maigizo ya kutumia mashairi, huwa kuna pande mbili unapinga na unaelewa jambo na mwisho kufikia muafaka.

VICHEKESHO

Ni maigizo mafupi ya kufurahisha hadhira

Mfano: -

- Mizengwe
- Original komedi
- Vituko show

FANI NA MAUDHUI

Kazi ya fasihi lazima iwe na fani na maudhui, vipengele hivi ni sura za falsafa moja si rahisi kuzitenganisha fani imo ndani ya maudhui.

FANI

Ni umbo la nje la kazi ya fasihi

MAUDHUI

Ni jambo analosema muandishi katika kazi yake ya fasihi

VIPENGELE VYA FANI

(i) Matumizi ya lugha

(ii) Mtindo

(iii) Muundo

(iv) Mandhari au mazingira

(v) Wahusika

(vi) Jina la kitabu.

MATUMIZI YA LUGHA

Msanii hutoa lugha kwa mpangilio maalumu wa maneno, tamathali za semi hutumiwa kwa upekee kulingana na mahitaji ya kazi hiyo.

MTINDO

Hii ni tabia ya pekee mtunzi katika simulizi au uandishi mtindo kutofautiana hali ya mtunzi na mtunzi.

MADHARI

Ni sura ya mahali mazingira ambapo kazi ya fasihi husika

WAHUSIKA

Ni watu, miti au viumbe hai vinavyowakilisha watendaji katika kuonyesha sifa za ndani na nje.

VIPENGELE VYA MAUDHUI

Kuna vipengele (5) vya maudhui navyo ni

(i) Dhamira

(ii) Ujumbe

(iii) Falsafa

(iv) Migogoro

(v) Mafunzo

DHAMIRA

Ni lengo la mtunzi wa kazi za fasihi. Mtunzi anaweza kutoa dhamira kuu na kujenga dhamira ndogondogo dhamira huweza kukosoa.

UJUMBE

Ni funzo analotoa mtunzi katika kazi ya fasihi kulingana na dhamira alizotoa

FALSAFA

Ni mawazo makuu ya mtunzi kuhusu maisha. Ni imani ya maandishi kuhusu maisha.

MIGOGORO

Ni hali ya kutoelewa na baina ya pande mbili au zaidi.

MAFUNZO

Ni mafunzo makuu ya mtunzi kuhusu maisha.wakati mwingine hadhira inaweza kupata mafunzo mabaya au mazuri kwa wahusika wakazi hiyo.

UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI

Maana;
Uhakiki ni kazi au kitendo cha kuchambua na kufafanua kazi ya fasihi ili kuweza kupata maadili na ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi.

au

Uhakiki ni sayansi maalum ya kuchambua kazi ya sanaa kwa undani na kuona ubora wa kazi ya fasihi kwa kutumia vipengele vya fani na maudhui na kuangalia uwiano na uhusiano wake na

jamii.

UMUHIMU WA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI

1. Kuchambua na kuweka wazi fumbo ambalo litapatikana na kazi ya fasihi.

2. Kuchambua na kufafanua picha za kisanii zilizotumika katika kazi ya fasihi.

3. Kumshauri mwandishi ili afanye kazi bora.

4. Kumuelekeza msomaji ili apate faida zaidi kuliko yale ambayo angeweza kuyapata bila dira ya muhakikiki (mhakiki ni mwalimu wa jamii)

5. Kuhimiza na kushirikisha fikra za kihakiki katika kazi za fasihi.

6. Kukuza kiwango cha utunzi na usomaji.

7. Kutafuta na kuweka sawa nadharia ya vitabu teule.

KUFAFANUA VIGEZO VYA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI.

1. Ukweli wa mambo yanayoelezwa.

2. Uhalisikaji wa watu, mazingira na matukio katika jamii.

3. Umuhimu wa kazi ya fasihi kwa jamii inayohusika lazima ufikiriwe.

UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI KATIKA FANI.

- Wahusika
- Mandhari
- Mtindo

MAUDHUI

- Ujumbe
- Mtindo

ZOEZI

1. Fasihi ni nini

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha ili kufikisha ujumbe kwa jamii fulani iliyokusudiwa

2. Orodhesha vipera vinne (4) vya semi na mfano

(i) Methali (kidole kimoja hakivunji chawa)

(ii) Mafumbo (uzalendo umemshinda)

(iii) Nahau (amepata jiko) – Ameoa

(iv) Vitendawili (uzi mwembamba umefunga dume) – Usingizi

3. Ainisha aina za maneno katika sentensi hii

Paka wale weusi walikuwa wanatembea ovyo barabarani

W TS T E

4. Taja matumizi mawili ya herufi kubwaa

(i) Hutumika kuandika jina, mahali ili kuleta maana .Mfano wa majina Asha, Ally Mfano wa mahali, Dar es salaam, Tanga n.k.

(ii) Hutumika mwanzo wa sentensi

USIMULIZI WA HADITHI

Usimulizi wa hadithi ni hali ya kueleza kitu au kuhadithia hadithi kwa njia ya mdomo.

MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA USIMULIZI WA HADITHI

(i) Kutumia lugha fasaha

(ii) Kuzingatia kiimbo

(iii) Matamshi

(iv) Mtiririko wa matukio ili walengwa waweze kuelewa kinachosimuliwa.

(v) Vitendo na maigizo ili kukwepa kuwachosha wasikilizaji

MASIMULIZI YA HADITHI

Ni masimulizi yenye lugha ya mjazo na mtiririko wake huwa sahihi au rahisi mara nyingi masimulizi ya hadithi huwa mafupi. Usimulizi ,utazamaji wa hadithi huwa na sifa kadhaa. Kinachotambulisha sifa hizo ni sehemu ya ambayo haiwezi kupotea au kupata pindi tusomapo kitabu.

Moja sauti ya mtambaji, msimulizi huusika moja kwa moja kwa hadithi

Utendaji wake jukwaani una nafasi kubwa ya hadhira. Utendaji huenda sambamba na lugha.

SIFA ZA UTENDAJI SIMULIZI

(i) Usemi halisi

(ii) Urudiaji

(iii) Sauti igizi

(iv) Matumizi ya viashiria

(v) Matumizi ya wakati

(vi) Uigizaji

1. **USEMI HALISI**

Msimulizi anasema moja kwa moja hadhira waweze kuelewa kwa urahisi na wasichoke kusikiliza.

2. **URUDIAJI**

Kama vipengele vingi vinavyorudiwa kama vile maneno, vifungu, nyimbo n.k

3. **SAUTI IGIZI**

Msimulizi anaweza kuiga sauti fulani kwa kutumia lugha inayomwezesha kubadilisha sauti yake katika fani mbalimbali.

4. **MATUMIZI YA VIAMBISHI**

Mtambaji hodari ana ufundi wa kutumia viashiria mbalimbali kukoleza usimulizi wake. Viashiria hivyo ni kama: -

- Mikono
- Mikunjo ya uso
- Mchezesho wa macho
- Viungo vingine vya mwili

5. **MATUMIZI YA WAKATI ULIOPO**

Wakati uliopo kihistoria au uliopita kisimulizi.

- Usimulizi huwa katika wakati uliopita lakini pia huchanganya sifa zinazohusisha wakati uliopo ilikuonesha umbali uliopo kati ya hadhira na simulizi umepunguzwa.

6. **UIGIZAJI**

Msimulizi wa hadithi anaiga sauti mbalimbali za wahusika au wanyama katika utambaji wake.

UANDISHI WA BARUA

BARUA

Ni maandishi yenye ujumbe yanayopelekwa kwa mtu mwingine kwa njia mbalimbali

Mfano wa njia hizo ni: -

- Posta
- Mkono
- Basi au ndege n.k

Kuna aina mbalimbali za barua kama vile: -

- Barua za kirafiki
- Barua rasmi
- Barua za mialiko
- Barua za kindugu

BARUA ZA KIRAFIKI

Hizi ni barua ziandikwazo kwa marafiki, jamaa, ndugu, wazazi.

LENGO LA BARUA ZA KIRAFIKI

1. Kusalimiana na ndugu zetu
2. Kuomba msaada
3. Kutoa pongezi, hongera au pole
4. Kuomba msamaha

MUUNDO WA BARUA ZA KIRAFIKI

Barua za kirafiki huundwa na mambo muhimu yafuatayo

1. Anuani ya mwandishi
2. Tarehe
3. Mwanzo wa barua
4. Mwisho wa barua
5. Jina la mwandishi.

(i) ANUANI YA MWANDISHI

- Huandikwa juu kwenye pembe ya kulia ya karatasi. Huandikwa kwa waziwazi na kwa usahihi ili mwandikiwa aitumie kujibu barua aliyotumiwa

- Huweza kuandikwa kwa muundo wa mshazari au wima.

MFANO WA MSHAZARI

SHULE YA SEKONDARI MAKONGO

S. L.P 60157

DAR ES SALAAM

19/07/2012

MFANO WA WIMA

SHULE YA SEKONDARI MAKONGO

S. L.P 60157

DAR ES SALAAM

19/07/2012

(ii) TAREHE

- Huandikwa chini kwenye anuani ya mwandishi ili kumjulisha mwandikiwa lini barua imeandikwa

- Tarehe huweza kuandikwa kwa miundo mbalimbali mfano: - 2-02-2012, 02/02/2012, 2.2.2012 au february

(iii) MWANZO WA BARUA

Huandikwa kushoto chini ya mstari wa tarehe huweza kuandikwa kwa kutajwa jina, eneo au wadhifa wa mtu anayeandikiwa

Mfano: -

Mpendwa Baba, mama, kaka, mpenzi wangu na pia sehemu hii kukaa maneno ya sehemu maamkizi ili kujulikana kati ya mwandishi na mwandikiwa

(iv) KIINI CHA BARUA

Sehemu hii hueleza kusudi/lengo la mwandishi, huelezea kusudi lake la kuandika barua.

Mfano: -

- Kuomba kazi
- Kuomba msaada
- Kuomba msamaha
- Kujuliana hali

(v) MWISHO WA BARUA

Hapa huwa na salamu za maagano na salamu hizo kutegemea mwandishi na mwandikiwa, mwisho wa barua huwa na maneno yenye ladha na mvuto.

Mfano: -

Wasalamu/ nisalimie wote wanaonifahamu nakusubiri kwa hamu n.k

(vi) JINA LA MWANDISHI

Ni muhimu mwandishi kuandika jina ili kumjulisha mwandikiwa barua imetoka kwa nani.

Angalizo: -

Uandishi wa barua za kirafiki hufuata taratibu zote za uandishi

Mfano:-

- Mkato
- Nukta
- Alama za kuuliza
- Mshangao n.k

KIELELEZO CHA MUUNDO WA BARUA ZA KIRAFIKI

SHULE YA SEKONDARI MAKONGO
S. L.P 60157
DAR ES SALAAM
19/07/2012

Baba mpendwa;

Salamu sana, je! Hamjambo wote hapo nyumbani? Wale mbuzi wangu mapacha niliowaacha wamezaa tena? Natumaini wadogo zangu kulwa na doto wanaendelea vema na masomo.

Dhima la barua hii ni kutaka kukujulisha maendeleo yangu ya shuleni ya kidato cha kwanza. Pia tatizo kubwa linaloniandama hapa shuleni ni umaskini sina hata shilingi moja ya kununua hata kipande cha mboga. Hivyo naomba nitumie hela ya matumizi ili nisome vizuri.

Wasalimie wote hapo nyumbani pamoja na marafiki zangu wote.

Wako akupendaye

ELIMUKAZI

UANDISHI WA INSHA

TARATIBU ZA UANDISHI

Alama na mpangilio wa maneno ni mojawapo ya vigezo vya kutambulisha mwandishi bora hodari kaziiwezekuwa nzuri inayoeleweka na wasomaji, mwandishi hana budi kutumia mfumo wa alama ili kumsaidia msomaji wapi pa kumpumzisha, kuuliza swali n.k baadhiya alama zifuatazo hutumika katika uandishi.

Mkato (,)

Alama hii hutumika

- kuweka pumziko fupi katika sentensi

- kutenga maneno yaliyo katika orodha

- huonyesha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume

Mfano: - Umoja ni nguvu, utengano ni dhaifu

NUKTA (.)

Alama hii hutumika

- kukamilisha sentensi

- kuonyesha ufupisho wa maneno

mfano: - R.T.D (Radio Tanzania Dar es salaam)

NUKTA MKATO (;)

Alama hii hutumika

Kuunga sentensi mbili zinazoweza kusimama zenyewe bila kutumia kiunganishi.

Mfano: -Hapo zamani za kale wazee walijiheshimi; sikuhizi hawajiheshimu.

Humpa msomaji pumziko fupi katika sentensi.

NUKTA/ NUKTA PACHA(:)

Alama hii hutumika

- kuunga sentensi mbili zinazoweza kusema zenyewe, bila kutumia kiunganishi

- kuunga/kuonesha vitu vilivyo katika orodha

mfano: - Nilileta vitu hivi: wino, karatasi, embe, ndizi na nanasi.

ALAMA YA MSHANGAO (!)

- Hutumika baada ya neno au usemi wa kushangaza au kushtuka

- Hutumika kuonesha msisitizo, kushangaa, kero n.k.

Mfano: - Hivi ni kweli! Mwone alivyo.

ALAMA YA KUULIZA (?)

Huonesha hali ya kuuliza swali katika tungo/ sentensi

Mfano: -

- Wanakuja saa ngapi?

- Wanamaana gani?

MABANO [( )]

Hutumika kuonesha maana ya ziada katika sentensi

Mfano: - Nchi yangu (Tanzania) naipenda sana

KISTARI (-)

Hutumika kuunda maneno

Mfano: - Ed-elfitr, Dar-es-salaam

Hutumika badala ya nukta mbili

Mfano: - tulipofika mbugani – tuliwaona swala wamelala – Swala dume na watoto watatu.

- Hutumika kuonesha kama neno limekatwa kwa kuwa limefika ukingoni.

ALAMA ZA MTAJO (“ ”)

Hutumika kuonesha maneno yaliyosemwa na mtu mwingine katika sentensi.

Mfano: - Nguchiro alisema " hakika mzee Ngwale ni katili sana"

Hutumika kubainisha maneno ya kigeni katika lugha nyingine.

Mfano: - (" **yes**") katika kiswahili.

UANDISHI WA INSHA

Insha ni kifungu cha habari chenye kueleza hoja au picha za mtu juu ya jambo fulani

- Insha hugawanywa katika vifungu, navyo ni: -
- Insha huweza kuwa na haya moja au wakili na kila haya hubeba wazo kuu moja matumizi
- Kuna aina kuu mbili za insha

(i) Insha za wasifu

(ii) Insha za hoja

INSHA

HIKI NI KIELELEZO CHA ISHA ZA HOJA NA WASIFU

- **INSHA ZA WASIFU**	- **INSHA ZA HOJA**
- Insha za wasifu za kisanaa - Insha za wasifu zisizo za kisanaa.	- Insha za hoja - Insha za kisanaa - Insha za hoja zisizo za kisanaa - Insha za wasifu

INSHA ZA HOJA

Hueleza mawazo fulani na hupanga mengine

Mifano ya vichwa vya insha vifuatavyo ni vya insha ya hoja.

- Elimu itolewe kwa watoto wa kiume tu.
- Shule za kutwa ni bora kuliko shule za bweni.

INSHA ZA WASIFU

Hii hueleza sifa za watu au vitu kama wanyama, milima, miti au mahali fulani: -

MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UANDISHI WA INSHA

1. **KICHWA CHA INSHA**

Huandikwa kwa herufi kubwa katikati juu ya insha

Huandikwa kwa ufasaha na kwa muhtasari

Kichwa kisizidi maneno matano(5)

2. **MWANZO WA INSHA**

Huzingatia tafsiri ya jambo linalozungumzwa, uhusiano wake na vitu vingine.

Kwa kawaida mwanzo huzidi aya moja

3. **KIINI CHA INSHA**

Hii ni sehemu kuu ya insha huzingatia mawazo makuu ambayo hupangwa katika haya zenye mtiririko mzuri wa mawazo.

Hueleza kwa undani juu ya jambo linalozungumzwa kwa uthibitisho.

4. **MWISHO WA INSHA**

Hutoa msisitizo kwa yaliyojadiliwa

Huonesha muhtasari wa yaliyojadiliwa na kuandikwa pamoja na hitimisho.

MAMBO YANAYOHITAJIKA KATIKA UTUNGAJI WA INSHA

1. Kichwa cha habari chenye kueleweka

2. Kuandika kwa kufuata kanuni na taratibu za uandishi

3. Kutumia lugha fasaha na rahisi.

4. Andika mwisho wa insha unaowavutia wasomaji au wasikilizaji.

INSHA KUHUSU MISITU

MISITU

Mimi naitwa Ajazi Mohamed natokea kijiji cha Njoro kilichopo Moshi mkoani Kilimanjaro. Katika kijiji hicho naishi na babu pamoja na bibi alikadhalika na ndugu zangu. Kila ifikapo jumamosi mimi na ndugu zangu huwa tunakwenda kukata kuni pia kuchuma matunda kama mananasi, maembe, machungwa pia maparachichi. Misitu husaidia kwa ajili ya kivuli, mvua pamoja na kuni. Pia misitu hiyo hiyo hutoa mbao kwa ajili ya kutengenezea vifaa vya nyumbani vikiwemo, meza, viti, makabati pamoja na vitanda. Pia mbao hutumika kujenga mapaa ya nyumba na kadhalika.

Misitu hiyohiyo hupenda kukaa wanyama wakali kama vile mbwa mwitu, nyoka na wadudu wenye sumu wakiwemo nyuki,dondola. Misitu ipo sehemu mbalimbali ikiwemo Moshi, Arusha, Songea pamoja na Singida. Misitu ni hatari sana hasa kwa watoto wadogo kwenda peke yao msituni au mwanamke kutembea peke yake jioni au usiku huwa ni hatari sana kwa sababu msituni kuna wanyama wakali sana na unaweza kukutana na majambazi.

Misitu ni muhimu kwa ajili ya mahitaji yetu ya nchi na ya nyumbani kwa ujumla pia tunasisitiza kutunza misitu, mazingira na maeneo tunayoishi.

TOFAUTI KATI YA INSHA ZA KISANAA NA ZISIZO ZA KISANAA

Insha za kisanaa
- Hizi ni Insha ambazo hutumia vipengele mbalimbali vya kifasihi katika kuwasilisha ujumbe. Mbinu hizo ni kama vile Nahau, Methali, Misemo, Tamathali za semi na mbinu nyingine za kisanaa.

Insha zisizo za kisanaa
- Hizi ni Insha ambazo hazitumii lugha ya kifasihi katika kufikisha ujumbe wake.

UFAHAMU

Ufahamu ni uwezo wa kuelewa jambo fulani na kuweza kulifafanua.

AINA ZA UFAHAMU

1. Ufahamu wa kusoma

2. Ufahamu wa kusikiliza

3. Ufahamu wa kutafakari

UFAHAMU WA KUSIKILIZA

- Ni kuzingatia yote yasemwayo na mtu mmoja, mwingine kusikiliza kunahitaji umakini na utulivu ili kuelewa.

- Watu huweza kupata taarifa kutokana na kusikiliza jambo husika kwa umakini na utulivu

Mfano: -

Mtoto akimsikiliza mwalimu kwa umakini huweza kufanya vizuri kwenye masomo. Hiyo kutokana na kumsikiliza mtu unaweza kupata maarifa, taarifa za kufurahisha/kuhuzunisha.

UFAHAMU KUHUSU KICHOCHO

Kichocho ni ugonjwa hatari sana , vilevile kichocho ni hatari katika jamii kiujumla. Pia kichocho kinaathiri wakubwa na watoto hasa wale wenye umri chini ya miaka 5,6 na 7.

Pia ugonjwa wa kichocho hutokana kwa njia mbalimbali ikiwemo kukojoa kwenye maji machafu, maji taka (mifereji)

UFAHAMU WA KUSOMA

Kusoma ni uwezo wa kuelewa maneno yaliyoandikwa. Ufahamu wa kusoma umegawanyika katika makundi mawili

- Kusoma kimya
- Kusoma kwa sauti

Msomaji anaweza kusoma kwa kutumia njia moja kati ya hizo mbili lengo ni kuelewa jambo au ujumbe aliosoma.

Katika kusoma mtu anaweza kupata maarifa/ ujumbe mbalimbali wa kufundisha au kuhuzunisha na hata msisimuko kutokana na yaliyosomwa.

DHIMA ZA UFAHAMU

1. Husaidia katika kuokoa muda

2. Husaidia katika kupunguza gharama

3. Husaidia kutoa taarifa kwa ufupi na kumwezesha mtu kufuata maagizo.

4. Husaidia sana kukuza, kuelewa miongoni mwa wanafunzi.

5. Huelimisha.

UFUPISHO WA HABARI

Ni hali ya kusoma au kusikiliza habari na hatimaye kuiandika au kusimulia kwa ufupi bila kupoteza maana yake ya msingi.

Ni kitendo cha kuelewa habari uliyosoma au kusikiliza kwa kifupi kwa kutumia maneno yako mwenyewe. Msomaji huchukua mawazo makuu ya habari aliyonayo kulinganisha pamoja na mawazo yake mwenyewe.

LENGO LA UFUPISHO WA HABARI

1. Ufupisho hutumika katika shughuli za kila siku

2. Husaidia katika kupata kuelewa na usikivu (msomaji, msikilizaji)

3. Hurahisisha habari hivyo kuokoa muda

4. Hutumika katika kuandaa ripoti mbalimbali.

5. Husaidia kudondoa hoja mbalimbali zinazotokana na hotuba na mihadhara.

MFANO WA HABARI

Baba na mama wanajishughulisha zaidi na masuala ya kilimo. Mazao ambayo hupanda ni kama vile mahindi, mtama, ulezi, uwele n.k

UFUPISHO WAKE

Wazazi wangu ni wakulima wa mazao ya nafaka.

ZOEZI

Fupisha habari ifuatayo kwa maneno yasiyopungua....

Tatizo la kweli la kidunia ya leo si umaskini kwa maana tunao ujuzi wa mali zinazotuwezesha kufuta umaskini huo. Tatizo lenyewe hasa ni mgawanyiko wa binadamu katika tabaka mbili: -

- Tabaka la mahitaji

- Tabaka la umaskini

Jambo hili ndilo linaloleta tatizo la vita na chuki kati ya watu.

UFUPISHO WAKE

Tatizo la tabaka mbili, tabaka la mahitaji na tabaka la umaskini.